

## AINA YA VITENDO VYA UNYANYASAJI WA KIJINSIA .

### 1. Unyanyasaji wa kimwili

Unyanyasaji wa kimwili mara nyingi hubeba vitendo vya mtu kupewa kipigo na kusababishiwa majeraha na maumivu, vile vile hujumuisha ukeketaji, ambao unaweza kupelekea kifo au maumivu makubwa.

### 2. Unyanyasaji wa kingono

Hujumuhisha kubakwa ikimaanisha ku-lazimishwa kufanya ngono au tendo la ndoa bila ridhaa. Pia kuwa na uhusiano wa kingono na mtoto chini ya miaka 18, kulingana na sheria ya makosa ya jinai inatambulika ni ubakaji na udhalilishaji. Pia Kumuingilia mwanawake au mwanaume kinyume cha maumbile ni unyanyasaji wa kingono.

### 3. Unyanyasaji wa kisaikolojia

Hujumuhisha kutishiwa kupigwa, kubakwa, kutukanwa, kutolewa maneno ya kufadhaisha, kunyang'anywa mali/fedha zako, kukataliwa tendo la ndoa n.k.

## NAFASI YA JAMII KATIKA KUTOKOMEZA UNYANYASAJI WA KIJINSIA.

Jamii itambe kuwa mwanamke anayo haki kama alivyo mwaume na kuzungumzia haki zao sio upendeleo wala kuwasaidia bali kuongeza fursa ya kupata haki zao, uhuru wa mawazo, kushikilia nyazifa za uongozi na kuheshimiwa utu wao kama wanadamu wengine.

1. Kukubali zana ya usawa bayana ya mwanamke na mwanaume
2. Kuwa na dhamiri ya kweli ya kutokomeza mila potofu zinazo mdidimiza mwanamke kimaendeleo kama kuwanyima kurithi mali za familia au ukoo, kuwakataza kwenda shule na kutoa mawazo yao.
3. Kuchangia katika kuwafikishia watuhumiwa wa vitendo vya unyanyasaji kijinsia mbele ya vyombo vya sheria.

Ili kuondokana na mfumo dume ambao ni sawa na ukatili, woga wa ushindani kimaendeleo kifikiria na chanzo kikubwa cha umaskini uli-okithili kwenye jamii nyingi za kiafrika ma-badiliko yanaitajika leo.

**IMEANDALIWA NA SMECAO FUND  
KWA UFADHILI WA BREAD FOR THE WORLD  
YA UJERUMANI.**

## SMECAO FUND

P.O.BOX 87, SAME-  
KILIMANJARO  
KITENGO CHA HAKI ZA  
BINADAMU NA JINSIA.

## MISI 16 YA KUTI HAI KURONGIA VACHE KUSU.

SIKU 16 ZA KUPINGA  
UNYANYASAJI WA  
KIJINSIA.

### KAULI MBIU.

**“Miaka 50 ya Uhuru  
pinga ukatili Imarisha  
Tanzania huru”.**

**NI MAMA YAKO, NI DADA  
YAKO, NI BIBI YAKO NI  
SHANGAZI YAKO NA NI RAFIKI  
YAKO TUSIMAME KWA  
PAMOJA TUMTETEE  
LEO!!!!!!**

## SIKU 16 ZA KUPINGA UNYANYASAJI WA KIJINSIA NI NINI?

Siku 16 za kupinga unyanyasaji wa kijinsia ni kampeni ya kimataifa duniani kote iliyoanzishwa na kongamano lililoitishwa na Taasisi ya Uongozi wa Wanawake Ulimwengini mwaka 1991, wakikubaliana kuanzisha maadhimisho ya kimataifa ya kupinga unyanyasaji wa mwanamke kila ifikapo tar 25 novemba mpaka tarehe 10 Decemba kila mwaka ili kusisitiza uhusiano uliopo kati ya unyanyasaji wa wanawake na ukiukwaji wa Haki za Binadamu.

Siku hizi 16 hujumuhisha maadhimisho ya siku muhimu kama zifuatazo :

1. NOV 29 - Siku ya kupigania Haki za Binadamu za mwanamke Duniani
2. DEC 1 - Siku ya Ukimwi Duniani na
3. DEC 10 Siku ya Haki za Binadamu Duniani

## UNYANYASAJI WA KIJINSIA NI NINI?

Unyanyasaji wa kijinsia ni tendo au matendo ya kutesa atendewayo mtu kinyume na matakwa/hiari ya mtu binafsi yakilingana na kutofautisha uhusiano kati ya mwanamke na mwanaume.

Na unyanyasaji huu huchukua sura tatu ambazo ni:

1. Unyanyasaji wa kimwili mfano Kupigwa
2. Unyanyasaji wa Kingono mfano Kubakwa
3. Unyanyasaji wa kisaikolojia mfano kutukanwa na kudhalilishwa utu.

Unyanyasaji hauangalii kabila, elimu, kipato/tabaka, utaifa, ukoo wala familia hutendeka kila mahali duniani na mara nyingi wanawake ndio wahanga wakubwa wa matendo haya ya unyanyasaji.

Inathibitishwa kuwa wanawake ni waathirika wakubwa wa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia Tanzania kutokana na Utafiti wa Shirika la Afya Duniani unaonyesha Kuwa asilimia 60 ya wanawake Tanzania walikubaliana na sababu moja au mbili zinazosababisha vitendo vya waume zao kuwapiga km Kubishana na mumeo

na n.k

## NINI KIFANYIKE VITENDO HIVI VIKITOKEA!

Aina yoyote ya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia unapotokea, kuna umuhimu mkubwa kumtaarifu mtu aliye karibu nawe unaye mwamini, pia inakupasa uvunje ukimya kama kuna nia ya kuleta mabadiliko. Hivyo inakupasa kutoa taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu nawe au ofisi za serikali ya kijiji na ofisi za kata ili mhusika achukuliwe hatua za kisheria.

Na vile vile unaweza wasiliana na Asasi ya Kijamii iliyo karibu nawe kama SMECAO.

Tukumbuke kuwa Unyanyasaji wowote wa kijinsia ni ukiukwaji wa sheria na uvunjaji wa misingi ya Haki za Binadamu na pia ni kwenda kinyume na sheria mama ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni Katiba ya nchi kwani inatamka sehemu ya tatu-Haki ya Usawa kuwa

*“Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa. Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake. Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria”.*